# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.15 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) MEI 2022

# RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AMWAGA AJIRA SEKTA YA ELIMU, AFYA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan*

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# UMAKINI UNAHITAJIKA KUJAZA NA KUTUMA MAOMBI YA AJIRA

Hivi karibuni Serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) imetoa tangazo la ajira za Walimu 9,800 pamoja na wahudumu wa Afya 7,612 ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na watumishi wa Afya katika Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati.

Kwa upade wa Kada ya Ualimu, limeainisha sifa na vigezo vya wanaohitajika katika ajira hizo huku ikisisitizwa kuwa wanaohusika ni wale waliohitimu Kozi za Ualimu kuanzia mwaka 2015 hadi 2021.

Tofauti na utaratibu wa zamani wa kuwasilisha maombi kwa mkono au kwa njia ya posta, utaratibu wa hivi karibuni unatumia mifumo ya kitehama ambapo walimu wenye sifa wanatakiwa kutuma maombi yao kupitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz.

Katika matumizi haya ya TEHAMA ni vizuri kila anayeomba kuongeza umakini na kuhakikisha kila sehemu anayotakiwa kujaza taarifa amejaza kwa usahihi, sehemu za kuweka vyeti aweke kile kinachohitajika na ahakikishe maombi yamekwenda.

Mwalimu anaweza akajaza taarifa zake kwa usahihi na kuzituma na akafikiri kwamba zimefika bila kujiridhisha kwamba mifumo hii inategemea uwepo wa intaneti katika ubora unaofaa. Sote tunajua kwamba katika maeneo yetu tunaweza kupata changamoto ya intaneti kutokuwa sawa au kuwa na spidi ndogo kwa muda fulani. Hivyo, ni vyema kujiridhisha kuwa mtandao unaotumia kwa muda huo upo sawa sawa na umezipakia taarifa zote na umezituma.

Mwisho, ni vyema tukumbushane pia kwamba maombi haya ni bure na hakuna upendeleo wa rushwa ya aina yoyote kwa ajili ya kupata ajira hizi. Hivyo, kila mmoja awe makini na kuepuka matapeli wanaoweza kukudanganya kwa namna yoyote ile. Na endapo ikitokea mtumishi au mtu yeyote anaomba au anatoa rushwa kwa ajili ya kupata ajira tafadhali toa taarifa kwa mamlaka zinazohusika ili hatua zichukuliwe mara moja. Rushwa ni adui wa Haki.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AMWAGA AJIRA SEKTA YA ELIMU, AFYA

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Katika juhudi za kuimarisha Sekta ya Elimu na Afya, Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kuajiri walimu 9,800 pamoja na wahudumu wa Afya 7,612 ili kukabiliana na upungufu wa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na watumishi wa Afya katika Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati.

Hilo limewekwa wazi kufuatia tangazo la nafasi za Ajira kwa Kada za Ualimu na Afya lililotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) tarehe 20 Aprili, 2022 likieleza kuwa TAMISEMI imepata kibali cha ajira za watumishi wa Kada hizo.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, wahitimu kutoka kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Afya vinavyotambuliwa na Serikali wanaweza kutuma maombi ya kazi kuanzia tarehe 20 Aprili – 04 Mei, 2022 ambapo nafasi hizo ni kwa wahitimu wa Astashahada (Certificate), Stashahada (Diploma) na Shahada (Degree).

Kuhusu taratibu za kuomba ajira za ualimu, Katibu Mkuu huyo alieleza kuwa walimu wote wenye sifa watume maombi yao kupitia kiunganishi cha ajira. tamisemi.go.tz huku ikisisitizwa kuwa tangazo hilo linawahusu wahitimu wa Kozi za Ualimu wa kuanzia mwaka 2015 hadi 2021.

Akifafanua sifa za Kitaaluma kwa walimu wanaoomba kufundisha shule za Msingi, Katibu Mkuu huyo alisema kuwa Mwalimu Daraja la III A anatakiwa kuwa na Astashahada ya Ualimu ya Msingi huku Mwalimu Daraja la II B anatakiwa kuwa na Stashahada ya ualimu wa Elimu ya Awali au ya Msingi.

Vilevile, Mwalimu Daraja la III C anatakiwa mwenye Shahada ya Ualimu kwa Elimu ya Awali na Mwalimu Daraja la III A, III B na III C awe mwenye Astashahada, Stashahada na Shahada ya Ualimu (Elimu Maalum) kwa masomo ya Lugha na Sanaa.

Kwa upande wa Sekondari, Mwalimu Daraja la III B anatakiwa mwenye Stashahada (Diploma) ya Ualimu aliyesomea Elimu Maalum kwa masomo ya English Language, Geography, History, Kiswahili, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics; Mwalimu Daraja la III C anatakiwa mwenye Shahada ya Ualimu aliyesomea Elimu Maalum kwa masomo ya English Language, Geography, History, Kiswahili, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics; Mwalimu Daraja la III B anatakiwa mwenye Stashahada ya Ualimu wa somo la Biology, Chemistry, Physics na Basic Mathematics; na Mwalimu Daraja la III C - Mwenye Shahada ya Ualimu somo la Physics, Mathematics, Chemistry



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe.*

# RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AMWAGA AJIRA SEKTA YA ELIMU, AFYA

na Biology.


Aidha, Mwalimu Daraja la III C anatakiwa mwenye Shahada ya Ualimu wa somo la English Language, English Literature, Chinese Language, French Language na Kiswahili; Mwalimu Daraja la III C - mwenye Shahada ya Ualimu somo la Commerce, Accountancy na Economics; Mwalimu Daraja la III B - mwenye Stashahada ya Ualimu Elimu somo la Book Keeping na Commerce na Mwalimu Daraja la III C - mwenye Shahada ya Ualimu kwa masomo ya General Studies, History na Geography.

Tangazo hilo liliendelea kueleza kuwa Mwalimu Daraja la III B - mwenye Stashahada ya Ualimu kwa masomo ya Civics, History, Geography, English Language na Kiswahili; Mwalimu Daraja la III C – mwenye Shahada ya Elimu ya Michezo (Bachelor of Science in/ with Physical Education); na Mwalimu Daraja la III B - mwenye Stashahada ya Elimu ya Michezo (Diploma in Physical Education).

Tangazo hili lilibainisha kuwa waombaji wote ni lazima wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri/Vituo watakavyopangiwa; wawe tayari kufanya kazi na Mashirika au Taasisi zilizoingia Ubia na Serikali; Baada ya kupangiwa kituo cha kazi, hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa kituo cha kazi; Waombaji wote wahakikishe wanajaza taarifa zao na kuambatisha nyaraka zote muhimu katika mfumo; na Maombi ya ajira ni bure.

Waombaji wote waliosoma Elimu ya Sekondari nje ya nchi wanatakiwa kupata Namba ya Ulinganifu wa Matokeo (Equivalent Number) inayoanza na Herufi EQ… kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania ili kuwawezesha kuingia kwenye Mfumo wa Ajira; na waombaji waliosoma Vyuo vya Nje ya Nchi wanatakiwa kupata Ithibati ya masomo yao kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili vyeti vyao viweze kutambuliwa na kupata uhalali wa kutumika hapa nchini.

Tangazo hilo pia lilibainisha kuwa, waombaji wenye Ulemavu na sifa zilizoainishwa watume maombi yao ya kazi kwa nakala ngumu wakieleza aina ya ulemavu wao na kuambatisha picha zao na kuyatuma kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira & Wenye Ulemavu).



# BAJETI YA TSC YAENDELEA KUONGEZEKA



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Innocent Bashungwa (kushoto) akipongezana na Katibu Mkuu wa OR – TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe mara baada ya Bajeti ya Ofisi hiyo kupitishwa na Bunge hivi karibuni.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Shilingi Trilioni 8.78 kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 184 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23 hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Innocent Bashungwa alisema kuwa kati ya fedha zinazoombwa, Shilingi Trilioni 5.51 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara Shilingi Trilioni 4.63 na Trilioni 0.88 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Aliendelea kufafanua mchanganuo wa fedha hizo alisema kuwa jumla ya Shilingi Trilioni 3.27 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo 2.15 ni fedha za ndani na Shilingi Trilioni 1.12 ni fedha za nje.

Akiizungumzia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Waziri huyo alisema TSC imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria Sura 448, Kanuni za Mwaka, 2016, Taratibu na miongozo inayohusu kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu nchini huku akieleza kuwa kutokana na uzito na umuhimu wa majukumu hayo Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya Tume hiyo kila mwaka.

"Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuiongezea Tume Bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 Tume ilitengewa Shilingi bilioni 4.62, mwaka wa fedha 2019/20 Shilingi bilioni 6.00, Mwaka wa fedha 2020/21 Shilingi bilioni 6.10 na mwaka wa fedha 2021/22 Tume ilitengewa Shilingi bilioni 6.60," alisema.

Waziri Bashungwa alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 TSC imetengewa Shilingi bilioni 6.70 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi. Aidha, Tume imetengewa Shilingi milioni



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Innocent Bashungwa (wa sita kutoka kulia mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi balimbali wa OR – TAMISEMI nje ya bunge mara baada ya Bajeti ya Ofisi hiyo kupitishwa na Bunge hivi karibuni.*

# BAJETI YA TSC YAENDELEA KUONGEZEKA

670.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Tume Makao Makuu na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa TSC- MIS.

Akizungumzia mafanikio ya TSC kwa mwaka wa fedha 2021/22 Waziri huyo alisema Dhima ya Tume ya Utumishi wa Walimu ni kuhakikisha walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Tanzania bara wanapata huduma bora kuhusu masuala ya ajira, kupandishwa vyeo na kukuza maadili katika Utumishi wa walimu.

"Katika kutekeleza Dhima hiyo, walimu 6,949 kati yao walimu 3,949 wa Shule za Msingi na walimu 3,000 wa Shule za Sekondari walioajiriwa mwezi Juni, 2021 walisajiliwa na kupewa namba za TSC, Walimu 591 walipewa vibali vya kustaafu, mikutano 223 ya Kisheria imefanyika kati ya mikutano 278 iliyopangwa kufanyika kwa mwaka," alisema.

Aliendelea kusema, "katika mikutano hiyo ya kisheria iliyofanyika, Walimu 1,872 walipandishwa vyeo ambapo walimu 914 wa shule za msingi na 958 wa shule za sekondari; walimu 222 walithibitishwa kazini na walimu 460 walibadilishiwa vyeo. Vilevile, mashauri ya kinidhamu ya walimu 642 kati ya 793 yalihitimishwa, na mashauri ya walimu 151 yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji."

"Aidha, hadi Februari, 2022 rufaa za walimu 147 kati ya rufaa 152 zilitolewa uamuzi na Tume. Pia, malalamiko ya walimu 405 kuhusu upandishwaji vyeo, ubadilishwaji vyeo na mashauri ya kinidhamu yalipokelewa na kushughulikiwa".

Kuhusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume hiyo, Bashungwa alisema kuwa mradi huo umeanza kutekelezwa katika eneo la Njedengwa, Dodoma na utakaogharimu Shilingi bilioni 3.86 hadi kukamilika na kueleza kuwa katika mwaka wa Fedha 2021/22 jumla ya Shilingi milioni 500 ziliidhinishwa, hadi Februari 2022, Shilingi milioni 500 zimepokelewa ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 386 zimetumika kumlipa Mkandarasi SUMA – JKT ikiwa ni malipo ya awali.

Vilevile, alisema kuwa TSC imesaidia kupunguza kero na malalamiko ya walimu nchini ambapo tathmini iliyofanywa imeonesha kwamba asilimia 69 ya wadau hasa walimu wanaridhishwa na huduma zinatolewa na Tume hiyo huku akisema ajira za walimu zimepanda kutoka 10,629 mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia 14,949 mwaka 2020/21 walimu 126,346 walipandishwa vyeo mwaka 2020/21 na Serikali inaendelea kushughulikia walimu 23,457 ambao wamechelewa kupandishwa vyeo kutokana na sababu mbalimbali. Aidha Kamati za Wilaya 139 zimejengewa uwezo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Mheshimiwa Spika, katika kushughulika kero za wastaafu, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanzisha dawati maalumu la kupokea malalamiko na kero za wastaafu. Aidha, Tume inaendelea na ujenzi wa Mfumo



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto) pamoja na viongozi wengine wakiwa nje ya ukumbi wa Bunge mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya OR – TAMISEMI ambayo inajumuisha bajeti ya TSC.*

wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Masuala ya Walimu (Teachers Service Commission Management Information System TSC-MIS) ambao utasaidia kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu," alisema.

Pamoja na mafanikio hayo, Waziri Bashungwa alieleza kuwa TSC katika kutekeleza majukumu yake imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali za walimu ikiwemo: upungufu wa walimu 100,958 wa shule za msingi na walimu 74,743 wa shule za sekondari hususan masomo ya sayansi; malalamiko ya walimu ikiwemo kutopandishwa vyeo kwa wakati; na wastaafu kucheleweshewa kulipwa stahili na mafao yao baada ya kustaafu.

# TSC YATOA MAFUNZO ELEKEZI KWA WAJUMBE WA KAMATI ZA WILAYA WA KANDA YA KASKAZINI NA KUSINI



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa hotuba ya ufunguzi wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendesha mafunzo elekezi ya wajumbe wa Kamati za Wilaya za Kanda ya Kaskazini na Kusini ikiwa ni hitimisho la kufanya mafunzo ya wajumbe wa kamati hizo katika Ofisi zote za Wilaya 139 za Tanzania Bara.

Mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati hizo ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 Kamati za Wilaya ndizo zenye mamlaka ya kuamua masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali.

Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 hadi 6, 2022 jijini Dodoma yalifunguliwa na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba ambaye alisisitiza wajumbe kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na kuhakikisha wanatenda haki katika kuamua masuala mbalimbali ya walimu.

Alifafanua kuwa kumekuwa na rufaa mbalimbali zinazokatwa na walimu kupinga maamuzi yaliyofanywa na Kamati za Wilaya ambapo baadhi ya rufaa hizo zinaonekana kutozingatia taratibu kitu ambacho kinasababisha Tume Makao Makuu kubatilisha uamuzi uliofanyika ngazi ya Wilaya.

"Nawaomba sana ndugu Wajumbe wa Kamati za Tume za Wilaya, tuzingatie sana Sheria, Kanuni na Taratibu katika utoaji maamuzi kwa mashauri mbalimbali ya nidhamu kwa Walimu, na pia ni vyema kujua na kuzingatia kuwa wakati mwingine yanawasilishwa mashauri ya nidhamu ambayo hayana mashiko mbele ya Tume. Tuwe makini sana katika maamuzi yetu, kama Kamati na tutende haki kwa Walimu wetu," alisema Prof. Komba.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa, Kamati za Wilaya zina wajibu wa kuhakikisha walimu wanapata uelewa juu ya masuala yanayohusu utumishi wao ikiwa ni pamoja na kutekeleza majukumu yao ya kufundisha wanafunzi kwa kuzingatia Miiko na Maadili ya Kazi hiyo ili waweze kuzalisha wanafunzi bora wenye tija kwa Taifa.

"Natoa wito kwenu Wajumbe wa Kamati za Tume Wilayani, muwe chachu ya kuliwezesha Taifa kuwa na watu waadilifu. Tutoe elimu na kuhamasisha uzalendo, uadilifu na diplomasia. Aidha, tutoe huduma na maamuzi kwa haki kwa awaye yeyote tunayemhudumia na hasa wateja wetu ambao ni walimu," Alisema Mwenyekiti huyo.

Akihitimisha hotuba yake ya ufunguzi, Prof. Komba aliwasihi washiriki wa mafunzo hayo kuwa wasikivu na kuzingatia yote watakayoelekezwa ili kuendeleza dhamira ya Tume na Serikali ya kuongeza ufanisi katika kuhudumia walimu.

"Mafunzo haya ndugu Wajumbe wa Kamati za Tume Wilayani yatatuwezesha kujua na kuelewa majukumu ya Tume na Kamati za Wilaya na hasa katika uwanda wa kushughulikia na kuendesha mashauri ya nidhamu pamoja na mambo mengine yanayohusu utumishi wa Walimu," alisema.

# TSC YATOA MAFUNZO ELEKEZI KWA WAJUMBE WA KAMATI ZA WILAYA WA KANDA YA KASKAZINI NA KUSINI



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akitoa neno la kumkaribisha Mwenyekiti wa TSC wakati wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya yaliyohusisha Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alisema kuwa pamoja na changamoto za kibajeti zinazoikabili tume hiyo, sulala la utoaji wa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati limepewa Kipaumbele kwani kamati hizo ndizo zinazoshughulika na walimu moja kwa moja.

"Pamoja na bajeti yetu kuwa ndogo, suala la kutoa mafunzo kwa kamati tumelipa msukumo mkubwa. Kwa mwaka huu wa fedha tulikuwa tumepanga kutoa mafunzo kwa kanda moja tu lakini kutokana na umuhimu tuliouona, leo hii tumefanya mafunzo katika Kanda tano, na hivyo tumemaliza kutoa mafunzo kwa Wilaya zote" alisema.

Nkwama aliongeza kuwa pamoja na kwamba wamefanya mafunzo kwa Kamati zote za Wilaya, wajumbe wawili tu kati ya watano kwa kila Wilaya ndio waliopata fursa ya kupata mafunzo hayo kutokana na changamoto za kibajeti na kuahidi kuwa pale ambapo bajeti itaruhusu mafunzo hayo yataendelea kutolewa kwa wajumbe waliobaki.

Katibu huyo aliongeza kuwa suala la kushughulikia maslahi ya watumishi wa umma wakiwemo walimu limepewa kipaumbele na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwani katika kipindi cha mwaka mmoja tangu aingie madarakani amemaliza kilio kilichokuwepo kwa muda mrefu cha walimu kutopandishwa vyeo.

"Moja ya mambo tunayojivunia na kumshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wake ni pamoja na kutuwezesha kupandisha vyeo Walimu wote waliostahili, jambo lililokua ni lalamiko kubwa la muda mrefu la Walimu. Hivyo, pamoja na malengo mengine, lengo kubwa la mafunzo haya kwa Kamati za TSC Wilayani ni kuendelea kuungana na Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha tunafikia adhma na malengo ya Serikali katika kuimarisha na kuboresha zaidi Sekta ya Elimu nchini," alisema Nkwama.

Katibu huyo pia aliwapongeza Wajumbe wa Kamati hizo kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kitu ambacho kimesababisha walimu kuendelea kufanya kazi kwa utulivu na kufanya kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuendelea kuongezeka.

"Wajumbe wote wa Kamati hizi za Wilaya ni Watumishi wa Umma ambao mna majukumu mengine ya kiutumishi. Licha ya majukumu mlionayo kwenye maeneo yenu ya kazi bado mmeonesha ushirikiano mkubwa na moyo wa kujituma katika kutekeleza majukumu ya Tume. Nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwaomba muendeleze moyo huo," alisema.

Mafunzo hayo yalihusisha wajumbe wa Kamati za TSC kutoka Wilaya za Mikoa ya Kilimajaro, Arusha, Ruvuma, Tanga, Mtwara na Lindi.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa kwenye mafunzo hayo zikiwemo; Kusudi la kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, Muundo na Majukumu ya Tume, Majukumu ya Tume kuhusu Ajira na Maendeleo ya Walimu, Maadili/ Miiko ya Kazi ya Ualimu, Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu na Taratibu za Uendeshaji wa vikao vya Kamati za Wilaya.



*Mshiriki wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini, Rhoda Masulende akitoa neno la shukrani kwa Mwenyekiti wa TSC (hayupo pichani) mara baada ya ufunguzi wa mafunzo hayo.*



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (kushoto) akiwa na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakiingia Ukumbini kwa ajili ya ufunguzi wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*









*Washiriki wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini wakiwa katika hali ya Utulivu wakati wa mafunzo hayo.*



*Mwenyekiti wa TSC, Willy Komba (kushoto) akiwa na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakifurahia jambo wakati wa ufunguzi wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu TSC, Mectildis Kapinga akiwasilisha mada juu ya Majukumu ya Tume kuhusu Ajira na Maendeleo ya Walimu wakati wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria TSC, Richard Odongo akiwasilisha mada kuhusu Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu wakati wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

















*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa kwanza upande wa kulia kutoka kwa mwenyekiti) pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# ZIFAHAMU KANUNI NANE ZA MWALIMU BORA



*Mwl. Robert Lwikolela, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Maadili na Nidhamu ya Walimu TSC.*

**Na Mwandishi Wetu**

Walimu wamekabidhiwa watoto shuleni na wanakuwa nao kwa kipindi kirefu zaidi wakati wa mchana, hivyo wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla wanategemea kwamba watoto watatunzwa, watafundishwa na kulelewa vizuri kitaaluma na kimaadili ili wawe raia wema na wenye tija kwa Taifa lao.

Hata hivyo, hii haina maana kwamba wazazi na jamii hawana wajibu wa kufanya katika kuwalea watoto bali kila upande unapaswa kutimiza wajibu wake kikamilifu ili watoto waweze kujengewa misingi bora wakiwa shuleni, nyumbani na hata mtaani wanapokutana na watu wa jamii tofauti tofauti.

Kutokana na jukumu hili zito na la kipekee alilopewa mwalimu linahitaji kujitoa na kufanya kazi kwa moyo, weledi na uadilifu wa hali ya juu ili kuwajengea watoto/wanafunzi msingi mzuri kwa ajili ya maisha yao ya baadae. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba mwalimu anatakiwa kuonesha kiwango cha kipekee cha tabia na maadili wakati wa utekelezaji wa kazi yake na kuwa kielelezo bora kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla.

Mwl. Robert Lwikolela ni Mkurugenzi Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) anayeshughulikia masuala ya Maadili na Nidhamu kwa walimu nchini, anabainisha kanuni nane za maadili ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma ambapo mwalimu ni miongoni mwa watumishi hao.

Kanuni ya kwanza ni kutoa huduma bora, Lwikolela anaeleza kuwa mwalimu au mtumishi yeyote wa umma anatakiwa kuepuka kuchelewesha huduma, kutoa huduma kwa heshima na kwa kumjali mteja. Mwalimu bora ni lazima awe na lugha nzuri, awe na staha pamoja na mavazi ya heshima yanayokubalika katika utumishi wa umma.

Pili ni utii kwa Serikali, Mkurugenzi Msaidizi huyo amesema kuwa mwalimu bora anatakiwa kutekeleza na kutimiza malengo yanayotolewa na viongozi wa kazi pamoja na kutii Serikali iliyoko madarakani na kamwe hapaswi kuwa kikwazo cha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa na serikali katika kutoa huduma kwa wananchi.

Mwalimu bora anatakiwa kuwa



*Mwalimu bora ni yule anayekamilisha kazi zake za kila siku kabla ya kuondoka ofisini.*

# ZIFAHAMU KANUNI NANE ZA MWALIMU BORA



*Mwalimu bora atafundisha kwa kutumia zana za kufundishia.*

na bidii ya kazi, hii inamaanisha kuwa mwalimu ni lazima ajali muda wa kazi kwa kufika kazini kwa wakati, kuondoka kazini baada ya kukamilisha majukumu aliyopaswa kufanya kwa siku hiyo, kutulia ofisini na kufanya kazi, kuwa tayari kufanya kazi katika kituo chochote cha kazi anachopangiwa na kutumia utaalamu, ujuzi na maarifa aliyonayo katika kuongeza tija kazini.

Vilevile, Mwalimu bora anatakiwa kutoa huduma bila upendeleo, hapa mwl. Lwikolea amesisitiza kuwa kwa mtumishi ambaye ni mwanachama wa chama cha siasa hapaswi kuchukua taarifa za Serikali na kuzipeleka kwenye chama chake, hatakiwi kuendekeza mambo ya siasa mahali pa kazi. Pia, ni mwiko kwa mtumishi wa umma kuendekeza udini au ukabia kazini au hata nje ya kazi.



*Mwalimu bora anahakikisha wanafunzi wake wameelewa kile alichowafundisha.*

# ZIFAHAMU KANUNI NANE ZA MWALIMU BORA



*Wanafunzi bora ni chachu ya maendeleo kwa jamii na Taifa kwa ujumla.*

Kanuni nyingine ni kufanya kazi kwa uadilifu na kuepuka matumizi mabaya ya madaraka na ofisi. Mtumishi bora anatakiwa kujali wateja, kuheshimu kazi, kuepuka kuwa na dharau, kusikiliza watumishi wenzake, kufanya kazi kwa kufuata taratibu, kutofanya kazi kwa mazoea, kuepuka vitendo vinavyoaibisha utumishi wa umma kama vile ulevi na matumizi ya dawa za kulevya, kuomba au kupokea rushwa pamoja na kuepuka mapenzi kazini, uzinzi na uasherati, kupigana, kusutana, kukopa hadi kushindwa kulipa, kutoheshimu mipaka ya kazi na unyanyasaji.

Pamoja na hayo, Mwl. Lwikolea amefafanua kanuni nyingine kuwa ni uwajibikaji kwa umma. Ameeleza kuwa mwalimu/mtumishi bora anapaswa kuwahudumia wateja na watumishi wenzake kwa heshima, kuwa makini wakati wa kuwahudumia wananchi wenye mahitaji maalamu pamoja na kutoa ufafanuzi juu ya taratibu za utoaji wa huduma za serikali kwa uwazi bila kujali muonekano wa mtu.

Kanuni ya saba ni kuheshimu sheria, mwalimu/mtumishi anatakiwa kufahamu sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya kazi. Pia, anatakiwa kutumia sheria na miongozo bila urasimu au kuchelewesha huduma pamoja na kutoa taarifa kwa Mamlaka kuhusu maagizo yanayokwenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu.

Mkurugenzi Msaidizi huyo amehitimisha kwa kufafanua kuwa mwalimu/mtumishi bora anatakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya taarifa. Hii inamaanisha kuwa mtumishi hapaswi kutoa taarifa za Serikali ziwe za siri au za kawaida bila kupewa idhini ya kufanya hivyo, kuepuka kuvujisha siri za serikali kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii au njia nyingine yoyote. Aidha, kila mtumishi anatakiwa kuzingatia Mwongozo wa matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini wa mwaka 2017.


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa
Kheri ya
MIAKA
58
YA MUUNGANO
1964 - 2022
Mwenyekiti, Makamishna , Menejimenti na Watumishi wote wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Tunawatakia Watanzania Kheri ya Sikukuu ya Muungano.
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# KAMATI ZA TSC ZATAKIWA KUSAIDIA WALIMU KUTATUA CHANGAMOTO ZAO



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Grace Magembe akifunga Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Inaelezwa kuwa moja ya changamoto zinazowakabili Watumishi wa Umma wakiwemo Walimu ni kukosa nafasi ya kusikilizwa na viongozi wao hasa pale wanapokabiliwa na changamoto binafsi kitu ambacho kinawasababishia msongo wa mawazo, kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi, kukata tamaa na hatimaye kujikuta wakiingia kwenye makosa ya kinidhamu.

Kutokana na hilo, watendaji wenye dhamana ya kusimamia walimu wametakiwa kuelekeza nguvu zao katika kuwasikiliza walimu na kusaidia kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili badala ya kukaa na kusubiri watende makosa ya kinidhamu ili wawachukulie hatua.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Katibu Mkuu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Grace Magembe wakati akifunga Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.

Dkt. Magembe alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imelenga kuwasaidia walimu kwa kuwawekea mazingira mazuri ili waweze kutoa huduma bora kwa wanafunzi, hivyo watendaji wenye dhamana ya kuwasimamia walimu hawana budi kuelekeza nguvu zao katika kutatua changamoto zao.

"Moja ya changamoto tulizonazo serikalini ni viongozi wenye dhamana ya kusimamia watumishi kutotaka kuwasikiliza. Yaani unakuta mwalimu ana shida anahangaika lakini akifika kwa kiongozi wake hasikilizwi badala yake ni kufokewa na kufukuzwa. Jambo hili linafanya watumishi kuwa na msongo wa mawazo, kukata tamaa na mwisho anaingia kwenye makosa ya kinidhamu na hatimaye anafukuzwa kazi, alisema Dkt. Magembe.

Alisema kuwa pamoja na kwamba Sheria, Kanuni na Taratibu zipo na ni lazima zizingatiwe, ni muhimu pia wenye dhamani kutumia utu, hekima na busara ili kuwasaidia walimu kutoingia kwenye makosa ya kinidhamu badala ya kukaa na kusubiri wafanye makosa ili wawachukulie hatua.

"Ninyi TSC mmepewa dhamana kubwa kushughulikia masuala ya utumishi wa walimu,



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akitoa neno la kumaribisha Naibu Katibu Mkuu kutoka OR – TAMISEMI, Dkt. Grace Magembe (hayupo pichani) ili afunge Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.*

# KAMATI ZA TSC ZATAKIWA KUSAIDIA WALIMU KUTATUA CHANGAMOTO ZAO

wasikilizeni walimu na wasaidieni kutatua changamoto zao. Kuna wengine unaweza kukuta wamechanganyikiwa kabisa na wamekata tamaa lakini kumbe ukiwasikiliza utakuta tatizo ni dogo tu, unakwenda kwa mkurugenzi wa halmashauri unamshauri mnamsaidia walimu mambo yakwenda vizuri. Kutafuta ufumbuzi wa changamoto za walimu ndiyo wajibu wenu," alisema.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja tangu aingie madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kuboresha elimu ikiwemo kujenga madarasa zaidi ya 15,000, kuajiri walimu zaidi ya 6,900, kupandisha madaraja walimu 126,346 na kuwabadilishia kazi/cheo walimu 11,363, hivyo Kamati hizo nazo zina wajibu wa kuunga mkono juhudi hizo kwa kutekeleleza wajibu wao kwa ufanisi.



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu kutoka OR – TAMISEMI, Dkt. Grace Magembe (kushoto), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (kulia) na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakizungumza jambo kabla ya kufunga Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.*

Dkt. Magembe alifafanua kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa vizuri hivyo ni lazima TSC ihakikishe kwamba walimu wanatulia kwenye vituo vyao vya kazi na wanafanya kazi wakiwa na amani na utulivu badala ya kuondoka vituoni kwenda kuhangaikia masuala yao ya kiutumishi.

Alisema TSC inatakiwa kuwa daraja kati ya walimu na ofisi mbalimbali za serikali zinazoshughulikia walimu na kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kila mwalimu anayewasilisha shida yake TSC aweze kupatiwa majibu kwa wakati.

"Tunataka kila mwalimu awe na uhakika kuwa akiwa na jambo lolote linalohusu utumishi wake akilifikisha TSC litafuatiliwa kikamilifu na kupatiwa ufumbuzi,

# KAMATI ZA TSC ZATAKIWA KUSAIDIA WALIMU KUTATUA CHANGAMOTO ZAO



*Washiriki wa Mafunzo wakiwa katika hali ya utulivu.*

hivyo hakuna haja kwa yeye kuondoka kituo chake cha kazi kwa ajili ya ufuatiliaji. Ni lazima msaidie kutetea maslahi ya walimu na kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa kwa haraka," alisema.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisisitiza kuwa Mamlaka ya Kamati za Wilaya yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 yanahitaji watu waadilifu na wanaosimamia haki bila kuogopa kwa kuwa yanahusisha kuamua hatma za ajira za walimu pamoja na maendeleo yao, hivyo wasipokuwa waadilifu walimu wataumia.

"Ninaamini ninyi ni waadilifu ndio maana mmeteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hizi. Sheria imewapa mamlaka ya kuamua hatma ya ajira ya mwalimu, mnaweza kutoa adhabu mbalimbali ikiwemo kufukuza kazi, kuamua mwalimu gani apande daraja na nani asipande, nk. Msipokuwa waadilifu hamtaweza kusimamia na kufanya maamuzi kwa haki na matokeo yake mtawaumiza walimu pamoja na wanaowategemea," alisema.

Naye Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alieleza kuwa TAMISEMI imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na TSC kitu ambacho kimesaidia changamoto mbalimbali za Tume hiyo kupatiwa ufumbuzi.

Hata hivyo, Prof. Komba alieleza kuwa pamoja na jitihada hizo kumekuwa na changamoto kwa upande wa ofisi za halmashauri ambazo zimekuwa ni kero kwa TSC na hivyo kuiomba TAMISEMI itoe maelekezo kwa wahusika ili ufumbuzi upatikane.

Alieleza kuwa moja ya changamoto hizo ni kitendo cha baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri kukataa kwa makusudi kutekeleza uamuzi unaotolewa na Tume ngazi ya



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Grace Magembe (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa tatu kutoka kulia kwa waliokaa), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto kwa waliokaa) pamoja na washiriki wa Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.*

# KAMATI ZA TSC ZATAKIWA KUSAIDIA WALIMU KUTATUA CHANGAMOTO ZAO

Wilaya kwa mashauri ya nidhamu ya walimu au TSC makao makuu kwa rufaa za walimu kitu ambacho ni ukiukwaji wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015.

"TSC ndiyo iliyopewa mamlaka ya kushughulikia nidhamu kwa walimu lakini cha kushangaza TSC inatoa uamuzi kwamba mwalimu hana hatia hivyo arudishwe kazini lakini unakuta mkurugenzi hataki kumrudisha na mwalimu anahangaika tu mtaani. Kwa kweli jambo hili ni baya na linakiuka haki ya mtumishi," alisema.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa changamoto nyingine ni waajiri kuwasimamishia mishahara au kuwaondoa kwenye orodha ya mishahara walimu hata kabla ya tuhuma zinazowakabili kufikishwa TSC na shauri kufunguliwa kama sheria inavyoelekeza kitu ambacho kimesababisha walimu kukosa haki yao ya kupata mshahara kwa mujibu wa taratibu.

"Changamoto ya tatu ndugu mgeni rasmi ni baadhi ya wajumbe wa kamati za TSC Wilaya hususan Katibu Tawala wa Wilaya na Afisa Elimu kutohudhuria wenyewe kwenye vikao vya Kamati na badala yake wanatuma wawakilishi. Unajua Wajumbe wote wameteuliwa kwa majina na sio kwa vyeo na wamekula kiapo cha kutekeleza majukumu hayo, kutuma mwakilishi sio sawa. Hilo nalo tunaomba mtusaidie kulitolea maelekezo," alisema Prof. Komba.

Akitoa neno la kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu huyo, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alisema mafunzo hayo yamehudhuriwa na wajumbe 103 kutoka Wilaya za Kanda ya Kaskazini na Kusini ambapo wilaya hizo zinakamilisha idadi ya wilaya zote 139 kupata mafunzo ya Kamati.

Pia, aliwapongeza wajumbe wa kamati hizo kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii na weledi licha ya kuwa kutopata mafunzo elekezi tangu walipoteuliwa katika nafasi hizo.

"Ndugu mgeni rasmi, wajumbe hawa waliteuliwa mwezi Mei, 2021 na katika kipindi chote wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa weledi licha ya kuwa tulikuwa hatujakutana nao hivi kuwapatia mafunzo elekezi. Nawapongeza kwani wamekuwa wakisoma sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo tumekuwa tukiwatumia katika kutekeleza majukumu yao," alisema Nkwama.



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Grace Magembe (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa tatu kutoka kulia kwa waliokaa), Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto kwa waliokaa) pamoja na washiriki wa Mafunzo Elekezi ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika kwa siku mbili, Aprili 5 na 6, 2022 jijini Dodoma.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akifungua kikao cha kupitia madodoso kwa ajili ya kufanya utafiti wa masuala ya utekelezaji wa majukumu ya TSC kilichofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa Jakaya Kiwete jijini Dodoma.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akichukua dondoo wakati wa kikao cha kupitia madodoso kwa ajili ya kufanya utafiti wa masuala ya utekelezaji wa majukumu ya TSC. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ukumbi wa Jakaya Kiwete jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini cha TSC, Evodia Pangani akitoa maneno ya utangulizi kuhusu utaratibu wa kupitia madodoso yaliyoandaliwa kwa lengo la kufanya utafiti wa masuala ya utekelezaji wa majukumu ya TSC.*



*Baadhi ya Wajumbe wa kikao cha kupitia madodoso kwa ajili ya kufanya utafiti wa masuala ya utekelezaji wa majukumu ya TSC wakiendelea na kikao.*

# HUZUNI, SIMANZI VYATANDA TSC KIFO CHA CHRISTIAN LUBINZA CLAVERY, AFISA TEHAMA

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Huzuni na simanzi vimewakumba watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kufuatia kifo cha mtumishi wa Tume hiyo, Christian Lubinza Clavery kilichotokea tarehe 14 Aprili, 2022 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mkoani Dar es Salaam.

Akizungumzia wasifu wa Marehemu katika hafla fupi ya kuaga mwili wa mtumishi huyo iliofanyika Aprili 16, 2022 katika Ofisi za TSC jijini Dodoma wakati wa Safari ya kusafirisha mwili wa marehemu kutoka Dar es Salaam kwenda Mkoani Mwanza, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alieleza kuwa TSC imepoteza mfanyakazi shupavu, mahiri, mwadilifu na mtu aliyekuwa na heshima kwa watu wote.

"Tume ya Utumishi wa Walimu inatambua na kupongeza mchango wa Christian katika kutekeleza majukumu yake ya kiofisi. Christian alikuwa mfanyakazi hodari, mwenye heshima kwa watu wote na rafiki wa kila mmoja wetu. Hakika Watumishi wa Tume tutaukosa uwepo wake na kumbukumbu alizotuachia hazitofutika milele,"



Picha ya Marehemu Christian Lubinza Clavery.



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akisoma wasifu wa Marehemu Christian Lubinza Clavery wakati wa hafla ya kuaga mwili huo iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC, Marehemu Christian Lubinza Clavery wakati wa hafla ya kuaga mwili huo iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*

# HUZUNI, SIMANZI VYATANDA TSC KIFO CHA CHRISTIAN LUBINZA CLAVERY, AFISA TEHAMA



*Katibu Mstaafu wa TSC, Winifrida Rutaindurwa akitoa salamu za rambirambi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC, Christian Lubinza Clavery iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Kamishna wa TSC, Zuzana Nussu akitoa salamu za rambirambi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC, Christian Lubinza Clavery iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*

alisema Nkwama.

Akizungumzia sababu za kifo cha mtumishi huyo, Nkwama alisema kuwa mnamo mwezi Mei, 2021 Christian aligundulika kuwa na maradhi ya Saratani ya Damu na katika vipindi tofauti aliendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Benjamin W. Mkapa – Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road – Dar es Salaam na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Dar es Salaam.

"Tume ya Utumishi wa Walimu imekuwa ikishirikiana na Familia ya Marehemu katika kufanikisha matibabu ya Christian. Aidha, kupitia Wizara ya Afya, Christian alipewa kibali cha kupatiwa matibabu zaidi nchini India kwa gharama za Serikali. Mipango ya kufanikisha safari ya India ilikuwa inaendelea na alitarajiwa kusafiri kwa ajili ya matibabu hayo kati ya tarehe 21 na 23 Aprili, 2022," alisema kiongozi huyo.

Aliendelea kusema, "kwa niaba ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, tunatoa pole kwa Familia ya Christian kwa kupoteza kijana wao mpendwa, tunazidi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa faraja na nguvu kuhimili pengo lake katika familia."

Naye Katibu Mstaafu wa TSC, Winifrida Rutaindurwa ambaye Marehemu Christian alianza kazi wakati wa uongozi wake alisema kuwa Marehemu alikuwa mtumishi mwenye nidhamu, aliyefanya kazi zake kwa weledi na



*Mmoja wanafamilia wa Marehemu Christian Lubinza Clavery akitoa neno la shukrani wakati wa hafla ya kuaga mwili wa Marehemu Christian iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC jijini Dodoma.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiongoza waombolezaji kuaga mwili wa Marehemu Christian Lubinza Clavery.*

# HUZUNI, SIMANZI VYATANDA TSC KIFO CHA CHRISTIAN LUBINZA CLAVERY, AFISA TEHAMA





*Baadhi ya watumishi wa TSC na waombolezaji wengine wakiwa katika hali ya huzuni wakati wa hafla ya kuaga mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC, Christian Lubinza Clavery iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*

kujituma kitu ambacho kiliifanya TSC kupiga hatua katika masuala ya matumizi ya TEHAMA.

"Kijana huyu aliajiriwa wakati nikiwa Katibu wa Tume, kwa kweli alikuwa na bidii na aliijali sana kazi yake. Alikuwa ni mtaalamu mzuri wa TEHAMA na aliisadia Tume kuimarisha mifumo yake na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli mbalimbali za kiofisi. Ninajua hata sasa bado alikuwa anahitajika sana lakini hatuna cha kufanya, tuendelee kumshukuru Mungu kwa muda aliotupa kuishi pamoja na ndugu yetu Christian," alisema Rutaindurwa.

Kwa upande wa familia ya Marehemu walishukuru kwa upendo, ushirikiano na uwajibikawa wa hali na mali uliooneshwa na TSC katika kipindi chote cha ugonjwa pamoja na msiba wa mtumishi huyo.

Baada ya hafla hiyo Safari ya kusafirisha mwili wa marehemu iliendelea ambapo baadhi ya watumishi wa TSC Makao Makuu waliambatana na msafari huo kuelekea Mkoani Mwanza kwa ajili ya shughuli za mazishi ambazo zilifanyika Jumatatu ya Aprili 18, 2022.

Katika Msiba huo, watumishi wa TSC kutoka Makao Makuu na wilayani waliendelea na utaratibu wao wa kutoa mchango wa rambirambi ambapo kiasi cha shilingi 4,232,300 kilikusanywa na kukabidhiwa kwa familia ya Marehemu Christian.

Wakiwasilisha mchango huo wa rambirambi nyumbani kwa familia ya marehemu Aprili 25, 2022, baadhi ya watumishi wa TSC wa Wilaya za Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Mwl. Fundikira




*Picha ya Marehemu Christian Lubinza Clavery pamoja na jeneza lililobeba mwili wake.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Utwala kutoka TSC, Apsa Othman akiwa katika hali ya majionzi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa aliyekuwa mtumishi wa TSC, Christian Lubinza Clavery iliyofanyika Aprili 16, 2022 katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*

# HUZUNI, SIMANZI VYATANDA TSC KIFO CHA CHRISTIAN LUBINZA CLAVERY, AFISA TEHAMA

James walisema kuwa familia hiyo imewashukuru watumishi wa TSC kwa moyo wa upendo waliouonesha katika msiba huo.

"Kwa ujumla familia inaishukuru sana jumuiya ya watumishi wa TSC kwa kuendelea kuwa nao karibu na kuwaonesha moyo wa upendo na kujali wakati wote wa msiba. Hivyo, ninawaomba ndugu wana TSC tuzidi kuikumbuka familia hii kwenye sala na maombi yetu," alisema Fundikira.

Marehemu Christian alizaliwa Desemba 23, 1994 katika Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza akiwa ni mtoto wa tatu kati ya watoto watatu wa Familia ya Bwana na Bibi Lubinza Clavery.

Marehemu alianza elimu ya msingi katika shule ya Msingi Nyang'omango mwaka 2002 hadi 2008 kisha alisoma Kidato cha Kwanza na cha Pili katika shule ya Sekondari Sanjao na baadae aliendelea na Kidato cha Tatu na cha Nne katika shule ya Sekondari Mwanza mwaka 2009 hadi 2012.



*Shughuli ya kuzika mwili wa Marehemu Christian Lubinza Clavery ikiwa inaendelea.*

Mwaka 2013, Marehemu alijiunga na Kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Bariadi ambapo alihitimu Kidato cha Sita mwaka 2015 na mwaka huo huo alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alisoma shada ya kwanza hadi mwaka 2018 alipohitimu na kutunukiwa Cheti cha shahada ya Kwanza katika Sayansi ya Kompyuta.

Marehemu Christian aliajiriwa katika Utumishi wa Umma mnamo tarehe 03 Julai, 2019 na kupangiwa kufanya kazi Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu (Makao Makuu) katika Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa cheo cha Afisa Tehema Daraja la Pili, cheo ambacho alikifanyia kazi mpaka alipofikwa na umauti.



*Baadhi ya Watumisi wa TSC wa Wilaya za Mkoa wa Mwanza wakiwa pamoja na wana familia wa Marehemu Christian Clavery nyumbani kwa mama wa marehemu Christian mkoani Mwanza. Watumishi hao walifika nyumbani kwa familia hiyo kwa lengo la kuwasilisha mchango wa rambirambi uliotolewa na watumishi wa TSC.*



*Baadhi ya Watumisi wa TSC wa Wilaya za Mkoa wa Mwanza wakiwa pamoja na wana familia wa Marehemu Christian Clavery nyumbani kwa mama wa marehemu Christian mkoani Mwanza. Watumishi hao walifika nyumbani kwa familia hiyo kwa lengo la kuwasilisha mchango wa rambirambi uliotolewa na watumishi wa TSC.*

# KAMATI ZA WILAYA ZAPEWA ELIMU MASUALA YA MASHAURI YA NIDHAMU, RUFAA, AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria TSC, Richard Odongo akiwasilisha mada kuhusu Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu wakati wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Washiriki wa Mafunzo elekezi ya wajumbe wa Kamati za Wilaya za Kanda ya Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma walipata fursa ya kupata elimu ya kina juu ya taratibu za masuala ya mashauri ya nidhamu, rufaa, ajira na maendeleo ya walimu.

Hayo yamebainika kutokana na mada zilizowasilishwa na mwanasheria nguli wa masuala ya utumishi wa umma ambaye pia ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Wakili Richard Odongo pamoja na Mkurugenzi Msaidiazi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga wote kutoka TSC Makao Makuu.

Wakili Odongo alianza kwa kueleza kuwa Kifungu cha 5(c) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, kinatamka kuwa Tume itakuwa Mamlaka ya Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walioko kwenye Utumishi wa Umma huku akifafanua kuwa Sheria hiyo imeweka mamlaka zake katika ngazi ya awali (Original Jurisdiction) na ngazi za Rufaa (Appellate Jurisdiction).

Alisema kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 12(3)(a) ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016, Mwalimu Mkuu ni Mamlaka ya nidhamu kwa mwalimu katika makosa ambayo adhabu zake ni pamoja na malipo ya fidia au sehemu ya hasara au uharibifu uliosababishwa na kutochukua hatua au uzembe, kusimamisha ongezeko la mshahara (increment), Karipio au Onyo.

"Ikiwa mtuhumiwa ni Mwalimu Mkuu au Mkuu wa Shule, Mamlaka yake ya Nidhamu kwa adhabu zilizotajwa hapo juu, itakuwa Kamati/ Mamlaka ya Nidhamu ngazi ya Wilaya kama mamlaka yake ya awali," alisema Odongo.

Alifafanua kuwa kwa mujibu wa Kanuni 12(2) ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016 Kamati ya Wilaya ni Mamlaka ya Nidhamu katika makosa ambayo adhabu zake ni moja kati ya: - kufukuzwa kazi, kushushwa cheo, kushushwa mshahara kwa asilimia 15 kwa muda wa miaka 3, au kusimamishwa kwa ongezeko la mshahara.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa katika kushughulikia mashauri ya nidhamu za Walimu, pale inapolazimu; Kamati za Wilaya zimepewa Mamlaka Kisheria kumhoji Mwajiri (Mkurugenzi wa Halmashauri) husika ili kupata yale ya upande wa pili kabla ya kufanya maamuzi na kutoa adhabu kwa Mwalimu huku akiwasisitiza wajumbe hao kuzingatia sheria na taratibu badala ya kufanya maamuzi kwa mihemko.

# KAMATI ZA WILAYA ZAPEWA ELIMU MASUALA YA MASHAURI YA NIDHAMU, RUFAA, AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu TSC, Mectildis Kapinga akiwasilisha mada juu ya Majukumu ya Tume kuhusu Ajira na Maendeleo ya Walimu wakati wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

"Ni lazima tutofautishe utekelezaji wa majukumu ya Umma na majukumu ya kifamilia. Tusiingize mihemko ya kifamilia na ile binafsi katika kuwahudumia Walimu wetu. Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu imeelezea kwa kina mamlaka za nidhamu katika ngazi tofauti ikiwemo Wilaya. Tuzingatie Sheria, Kanuni na Taratibu katika kuwahudumia Walimu na pia katika kushughulikia mashauri yao ya nidhamu," alisema Odongo.

Kiongozi huyo aliendelea kusema moja ya majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu ni kushughulikia rufaa za walimu kutoka kwenye Mamlaka za Nidhamu na kusema kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, Rais wa Nchi ndiyo Mamlaka ya mwisho ya Rufaa kwa Walimu katika mashauri ya nidhamu ya kiutumishi.

Akizungumzia masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Kapinga alisema kuwa TSC imepewa jukumu la kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu na kwa kuwa walimu wapo wilayani majukumu hayo kwa kiasi kikubwa hutekelezwa katika ofisi za Tume ngazi ya Wilaya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maelekezo yanayotolewa na Tume.

Alisema kuwa kutokana na majukumu hayo kutekelezwa Wilayani kwa kiasi kikubwa, wajibu wa TSC Makao Makuu ni kutoa ushauri kwenye ngazi ya Wilaya kuhusu masuala ya ajira na maendeleo ya walimu, kutoa ufafanuzi na maelekezo kwa ngazi ya wilaya juu ya sheria, kanuni, taratibu, miongozo na maelekezo yanayotolewa na serikali pamoja na kutunza rejesta ya walimu wote na kutoa namba za usajili kwa walimu wapya.

"Kazi nyingine ni kukagua na kuchambua TANGE za wilaya na kuzithibitisha, kufuatilia na kuwajengea uwezo watumishi kwenye Ofisi za Wilaya kuhusu masuala ya ajira, kupandisha vyeo, kubadilishia walimu kazi/cheo,uwiano sawa wa upangaji wa walimu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule, kutunza kumbukumbu za walimu wote kwenye majalada ya wazi na siri pamoja na kukokotoa mafao kwa walimu wa Mikataba au Mirathi ya kabla ya tarehe 1.7.2004 ambayo hayalipwi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii bali hulipwa na HAZINA," alisema Kapinga.

Kapinga alisema kuwa kazi zinazofanywa na ofisi za wilaya ni kuhakiki mikataba ya ajira iliyojazwa kazi ya mwalimu na mwajiri, kutoa barua za ajira zenye Masharti ya Kudumu na Malipo ya Uzeeni au masharti mengine, kutunza Rejesta za Usajili, kuandaa, kuhuisha na kutumia Tange sahihi ya walimu na kupendekeza kwa Tume

# KAMATI ZA WILAYA ZAPEWA ELIMU MASUALA YA MASHAURI YA NIDHAMU, RUFAA, AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU

kuajiriwa upya kwenye Utumishi wa Umma walimu ambao walifukuzwa/waliachishwa kazi na wamekuwa nje ya utumishi kwa muda usiopungua miezi 12.

Kwa mujibu wa Kapinga, majukumu mengine ya ofisi za Tume ngazi ya Wilaya ni kuthibitisha kazini walimu, kupandisha vyeo walimu, kuwabadilishia kazi/cheo walimu waliojiendeleza kielimu, kusimamia program za mafunzo kazini kwa walimu, kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa walimu ndani ya Serikali za Mitaa na shule pamoja na kushughulikia hitimisho la kazi ya ualimu.

Pamoja na mambo mengine aliyoyazungumza, Kapinga alihitimisha mada yake kwa kuwasisitiza washiriki hao kufanya kazi kwa bidii ili serikali iweze kufikia malengo yake katika kuboresha utumishi wa walimu nchini na huku akifafanua kuwa endapo kamati za Wilaya zitatekeleza wajibu wake ipasavyo, Tume Makao Makuu itakuwa imepunguziwa mzigo wa kushughulikia rufaa za walimu.

"Tume ina Imani na wajumbe wote wa Kamati za Wilaya. Hivyo, iwapo tutawajibika vizuri, tutaipunguzia Tume mzigo wa rufaa na malalamiko yanayowasilishwa na walimu. Ni vema Wajumbe wawe huru kuhoji na kuomba ufafanuzi ili kuelewa vizuri kabla ya kutoa uamuzi wowote kwenye vikao vya Kisheria." Alisema Kapinga.







*Washiriki wa Mafunzo ya Kamati za Wilaya kwa Kanda za Kaskazini na Kusini wakiwa katika hali ya Utulivu wakati wa mafunzo hayo.*

# TSC YASHIRIKI MICHEZO YA MEI MOSI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeungana na Taasisi zingine za Serikali kushiriki michezo ya Mei Mosi iliyofanyika kwa siku kadhaa katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma hivi karibuni.

Michezo hiyo imefanyika ikiwa ni maandalizi ya kuelekea katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yatakayofanyika kitaifa Jijini Dodoma ambapo mgeni rasmi ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Michuano hiyo iliyofunguliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthon Mtaka Aprili, 21, 2022 imehusisha michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa pete, kuvuta kamba, karata, kurusha tufe, riadha, bao, draft na baiskeli.

Mtaka, alisema kuwa Mkoa wa Dodoma umejipanga vizuri kuhakikisha kuwa shughuli hizo za Mei Mosi zinasaidia kuinua uchumi wa Mkoa huo huku akiwasisitiza wakazi wa Jiji hilo pamoja na wilaya jirani kutumia fursa ya michezo na maadhimisho ya Mei Mosi kufanya biashara ili kujiingizia kipato.

"Katika kufikia azma ya Serikali ya kuhakikisha kila fursa inayojitokeza inachangia ujenzi wa uchumi imara, Uongozi wa Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na wadau, umeazimia kutumia fursa ya Mei Mosi kitaifa kuziunganisha sekta zote za kiuchumi kwa manufaa mapana ya mkoa wetu na Taifa kwa ujumla," alisema Mtaka.

Katika ufunguzi wa Michezo




*Picha ya pamoja ya wanamichezo wa TSC wakiwa nje ya uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati wa maandamano ya michezo ya Mei Mosi yaliyofanyika Aprili 21, 2022.*



*Wanamichezo kutoka taasisi mbalimbali za Serikali wakiwa katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati wa ufunguzi wa michezo ya Mei Mosi iliyofanyika kwa siku kadhaa jijini Dodoma.*



*Wachezaji wa timu ya kuvuta kamba kutoka TSC wakijiweka tayari kuvuta kamba dhidi ya timu kutoka TARURA (hawapo pichani).*

# TSC YASHIRIKI MICHEZO YA MEI MOSI



*Mchezaji Sylver Igogo wa RST (mwenye namba 60 kifuani) akiwa pamoja na wachezaji wengine tayari kwa kuanza mbio za baiskeli.*

hiyo, wanamichezo walipata fursa ya kufanya maandamano kutoka katika viwanja vya Nyerere Square hadi kwenye uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma huku wakiwa na mabango yaliyotambulisha Wizara, Idara, Wakala, Mashirika, Mikoa na Halmashauri mbalimbali.

TSC imeshiriki mashindano hayo kwa kupeleka wachezaji wa michezo ya kuvuta kamba kwa upande wa wanaume, kuendesha baiskeli, karata, draft, bao pamoja na riadha ambapo licha ya kutoibuka na kombe kwenye mashindano hayo, timu za TSC zilionesha upinzani mkubwa na kiwango bora katika michezo mbalimbali iliyocheza.

Mashindano hayo yaliyofanyika kuanzia Aprili 16, 2022 yamefanyika kwa siku 14 ambapo yalihitimishwa rasmi tarehe Aprili, 2022 ikiwa ni siku moja kabla ya kufikia kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani.



*Mchezo wa karata ukiwa unaendelea ndani ya uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.*














*Wanamichezo wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa kwenye maadamano ya michezo ya Mei Mosi. Maandamano hayo yalifanyika Aprili 21, 2022 jijini Dodoma.*




**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu:** +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*